**NDIGANA KALI (EAST COAST FEVER)**

**Na Augustino Chengula**

**Utangulizi**

Ndigana Kali ni ugonjwa hatari unaowapata ng'ombe wenye sifa ya homa kali, kuvimba kwa matezi, upumuaji wa shida na vifo vingi hasa kwa ndama. Ng'ombe wa kienyeji hawapati kwa urahisi sana ugonjwa huu ukilinganisha na wale wa kisasa na hata madhara yake ni makubwa kwa ng'ombe wa kisasa. Ni ugonjwa unaoenezwa na kupe wanaojulikana kitaalamu kwa jina la '*Rhipicephalus appendiculatus'* wanao beba vijidudu vya ugonjwa vinavyoitwa *Theileria parva* kundi la protozoa. Kupe hawa ni wale wanaopatikana kwenye masikio la ng'ombe wakiwa na rangi ya kahawia (kupe sikio kahawia). Ugonjwa huu unapatikana zaidi katika maeneo yenye mvua nyingi na joto yanayowezesha kupe hawa kuishi.



Kupe aina ya *Rhipicephalus appendiculatus* (rangi ya kahawia) wanaobeba wadudu wa Ndigana Kali. Kushoto ni kupe wa kiume na kulia ni wa kike.



Hawa ni kupe wanao beba wadudu wa Ndigana kali wakilishambulia sikio kwa kupata chakula, wakati huo huo wadudu wa ugonjwa huacha na kuenda kwenye tezi ya karibu ya sikio (parotid) na kisha wadudu kusambaa mwili mzima.

Huu ni ugonjwa muhimu sana Afrika unaosababisha hasara kubwa sana kwa mfugaji inayotokana na vifo vya ngombe pamoja na gharama kubwa zinazotumika kukabiliana nao kama vile dawa ya kuogeshea na miundo mbinu yake, uchanjaji na gharama za matibabu. Ndigana Kali ni ugonjwa wa Afrika unaoyakumba maeneo mengi; Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Swaziland, Zimbabwe, Zambia, Tanzania, Kenya, na Uganda, Burundi, Rwanda, Malawi, Mozambique na Sudni Kusini. Ugonjwa huu uliweza kulipotiwa kwa mara ya kwanza nje ya Afrika katika visiwa vy Comoro mwaka 2003 na 2004 ukidhaniwa kupelekwa na ng’ombe kutoka Tanzania waliopelekwa kibiashara.

**Dalili za Ndigana Kali**

-Tangu kupe mwenye wadudu aume ng’ombe hadi kujitokeza kwa ugonjwa huchukua wastani wa siku 8 hadi 12; waweza kwenda hadi wiki 3.

-Dalili ya mwazno kabisa ya Ndigana Kali ni kuvimba kwa tezi lililo chini ya sikio (*parotid*) ambapo kupe wa ugonjwa hupata chakula. Hii inafuatiwa na kuvimba kwa matezi yote ya mwili na matezi yaliyo juu juu ndani ya ngozi kama la chini ya sikio na mabegani  yanaweza kuonekana kiurahisi na kugusika.

-Homa hujitokeza  (nyuzi joto 39.5 za sentigredi), huongezeka kwa ghafla na huendelea kuwepo wakati wote wa ugonjwa na inaweza kufikia nyuzi joto 42 za sentigredi.




-Kuonekana kwa damu kwenye ngozi ndani ya mdomo na macho; hupoteza hamu ya kula (maumivu mdomoni) na afya yake hudhofika kwa haraka sana.

-Machozi na makamasi vyaweza tiririka, upofu wa macho an kuharisha

-Mwishoni ng’ombe hupumua kwa shida kutokana na kujaa kwa maji ndani ya mapafu

-Kabla ya kifo ng’ombe huwa amelala chini, joto la mwili hushuka na mapovu mengi humtoka puani. Kifo mara nyingi hutokea baada ya siku 18-30 tangu ng’ombe aumwe na kupe mwenye wadudu wa ugonjwa.

-Ng’ombe wa kisasa wenye ugonjwa wanaweza kufa wote (asilimia 100)

-Ng’ombe wanaopona ugonjwa huu hasa ndama ukuaji wao huwa hafifu na wale wa maziwa hushindwa kutoa maziwa. Lakini huwa wamekingwa dhidi ya ugonjwa huu na wanaweza kuwa wasambazaji wa ugojnwa kwa ng’ombe wengine punde waumwapo na kupe.



Ng’ombe aliyekufa kwa Ndigana Kali na povu lililo mtoka kabla ya kufa kwake likionekana akiwa amekonda

**Ng’ombe akichinjwa**

-Matezi yote huwa yamevimba na yanaweza kuwa yamejaa hewa, damu au majimaji

-Mapovu kwenye mfumo wa upumuaji kuanzia puani, koromeo na kwenye mapafu

- Maji kwenye mapafu

Damu yaweza kuonekana kwenye kuta za mfumo wa chakula

**Magonjwa yanayofanana na Ndigana kali**

Ugonjwa wa Maji Moyo (Heartwarter), Nagana (Trypanosomiasis) Ugonjwa wa kukojoa damu (Babesiosis), Ndigana baridi (Anaplasmosis), Homa ya mapafu ya ng’ombe (Contagious bovine pleuropneumoniae).

**Utambuzi wa Ndigana Kali**

-Hufanywa kwa kutumia dalili zilizotajwa hapo juu kabla au za baada ya kuchinjwa

-Uthibitisho hufanywa kwa njia za kimaabara (Giemsa stain, ELISA and PCR).

**Upambanaji dhidi ya ugonjwa**

***Kinga-*** Kinga dhidi ya ugonjwa huu kwa miaka mingi sasa imekuwa ikifanywa kwa kutumia dawa (*acaricides*) kwenye majosho au pampu ili kuua kupe wanaoeneza wadudu wa ugonjwa huu. Hata hivyo njia hii bado haijaonyesha ufanisi kwa sababu ya gharama ya dawa kuwa kubwa sana kufanya wengi washindwe kuinunua, lakini pia uhaba wa majosho umechangia na kujibadilisha kwa wadudu wenyewe. Kwa sasa njia inayoonekana kufaa ni ile ya kutumia njia mbili kwa pamoja chanjo na kuogesha japo bado haijaenea maeneo mengi ya nchi.



Ng'ombe akichomwa sindano ya chanjo ya kukinga Ndigana Kali

**Matibabu**-Kwa sasa kuna aina tatu ya madawa yanayotumika kutibu Ndigana Kali; parvaquone (Clexon®) katika dosi ya 20 mg kwa kila kilo ya ngo'mbe kwenye misuli, buparvaquone (Butalex®) katika dosi ya 2.5 mg kwa kila kilo ya ng'ombe kwenye misuli mara mbili ikirudiwa baada ya masaa 48 na halofuginone lactate (Terit®). Fulosemide huongezwa endapo kutakuwa na maji kwenye mapafu.

**MAREJEO**

1. The Mecrk Veterinary Manual, Ninth Edition, Merck Sharp & Dohme Corp., a subsidiary of Merck & Co., Inc, Whitehouse Station, NJ, USA.

2. John Gachohi, Rob Skilton, Frank Hansen, Priscilla Ngumi na Philip Kitala, 2012. Epidemiology of East Coast fever (Theileria parva infection) in Kenya: past, present and the future. Parasites & Vectors 5:194

3. Office International des Epizooties (OIE) Technical Disease Cards, 2009. THEILERIOSIS